TANGAZO LA SERIKALI NA. 550 La Tarehe 26/07/2019.

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
(SURA NA 272)

AMRI

(Imetolewa kwa mujibu wa Kifungu Na.28(1)(d))

AMRI YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA KIBAIGWA ("KIBAIGWA WSSA"), LA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA), 2019

Kichwa cha Amri

1. Amri hii itajulikana kama, Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kibaigwa("Kibaigwa WSSA"), (la Kurekebisha Bei za Huduma za Maji safi na Usafi wa Mazingira), la Mwaka 2019.

Tarehe ya kuanza kutumika

2. Amri hii itachukuliwa kuanza kutumika rasmi kuanzia tarehe 1 Julai 2019.

Marekebisho ya bei

3. Bei za majisafi na usafi wa mazingira za Kibaigwa WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza katika Amri hii.

Masharti

4. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

(a) Kibaigwa WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Amri hii.

(b) Kibaigwa WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Amri hii.

(c) Kibaigwa WSSA itatekeleza Kifungu cha 43 cha Sheria ya EWURA na Kanuni ya sita (6) ya EWURA ya Taratibu za Kukusanya Ada na Toza iliyochapishwa katika Gazeti la Serikali Namba 193 la mwaka 2010.

(d) Kibaigwa WSSA itahakikisha ripoti zake za kifedha zinakaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) au taasisi yeyote ya ukaguzi wa

fedhailiyoidhinishwa kama kifungu cha 33 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma na kupeleka nakala za taarifa za kifedha zilizokaguliwa kwa EWURA.

(e) Ifikapo tarehe 30 Septemba 2019 au kabla, Kibaigwa WSSA itawasilisha EWURA Mpango wake wa Kibiashara (2019/20-2021/22) uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Agizo hili.

(f) Kibaigwa WSSA, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Amri za Bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Nne la Amri hii.

(g) Kibaigwa WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Kibaigwa WSSA ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake. Pia EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na Kibaigwa WSSA katika siku zijazo.

Agizo Na. 11-014 la tarehe 1 Juni, 2011

5. Amri hii inafuta Amri Na. 11-014 katika maeneo yanayohudumiwa na mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira yaKibaigwa (Kibaigwa WSSA).

MAJEDWALI

JEDWALI LA KWANZA

(Imetengenezwa chini ya Aya ya 3)

BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali 1.1: Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi/ Mita ya Ujazo)

Makundi ya Wateja	Makundi ya Matumizi	Bei za Sasa	Bei Zilizoidhnishwa		
		2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumani	0-25	1,500	1,480	1,530	1,590
	25above	1,500	1,490	1,540	1,600
Taasisi	-	1,500	1,500	1,550	1,610
Biashara		1,500	1,600	1,620	1,630
Magati		1,500	1,500	1,500	1,500

Jedwali 1.2:Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Maunganisho Mapya (TZS/Unganisho)

Kundi la Mteja	Ada ya Sasa	Ada Iliyoidhinishwa		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani	Asilimia ishirini ya gharama za maunganisho kama inavyojieleza katika Kifungu cha 24 cha Kanuni za Maji za 2013	Asilimia ishirini ya gharama za maunganisho kama inavyojieleza katika Kifungu cha 24 cha Kanuni za Maji za 2013		
Taasisi				
Biashara				
Magati				

Jedwali 1.3:Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Marejesho ya Huduma ya Maji Baada ya Kukatiwa (TZS/Rejesho)

Kundi la Mteja	Ada za Sasa	Ada Zilizoidhinishwa		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani	10,000	10,000	10,000	10,000
Taasisi	10,000	10,000	10,000	10,000
Biashara	10,000	10,000	10,000	10,000
Magati	10,000	10,000	10,000	10,000

JEDWALI LA PILI

(Imetengenezwa chini ya Aya ya 4(a))

MIRADI ITAKAYOTOKELEZWA (SH)

Na	Maelezo	2019/20	2020/21	2021/22
	Kukarabati na Kubadilisha			
1	Kufanya ukarabati wanyumba 2 za mashine zilizopo Ndurugumi na Kisima cha zamani.	1,500,000	0	0
2	Kufanya ubadilishaji wa pamp chakavu na kufunga mpya zenye kipimo cha 39kw na 7.5kw kwa visima vya mbuyuni na ndurugumi.	10,000,000	15,000,000	30,000,000
3	Kufanya ukarabati wa jengo la karakana	0	1,000,000	0
4	Kufanya ukarabati wa matenki mawili ya St Pio na Ndurugum	0	1,000,000	0
	Jumla ndogo	11,500,000	17,000,000	30,000,000
5	Ununuzi wa eneo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji katika eneo la Kinangali	5,000,000	0	0
6	Umaliziaji wa jengo la ofisi kwa kufanya kazi zifuatazo ,upauaji,umiminaji wa jamvi,upigaji wa plasta kuta za ndani na nje kupiga mbao za dali ,kufunga mbao za dali,kufitiha flem za milango,kufitisha madilisha ya vioo,kuweka sakafu ya vigae,kufitisha shata za milnga ya mbao na upigaji wa rangi kwenye dari na kuta.	15,000,000	15,000,000	0
7	Kufanya utafiti wa upatianaji maji chini ya aridhi ,uchimbaji wa kisima kirefu 1 ,ufungaji wa pamp ,ujenzi wa nyumba ya mashine na uunganishaji wa umeme wa TANESCO.	3,000,000	20,000,000	10,000,000
8	Uchimbaji na ununzi wa mabomba urefu wa km4 yenye kipenyo cha mm100 -mm63 kwa ajili ya kupandishia maji tankin na kusambazia maji kwa wateja katika eneo la Kidongo chekundu	0	18,000,000	20,000,000
9	Ununuzi wa mita 750 za malipo ya baada zenye kipenyo cha 3/4" pia mita kubwa 5 za kwenye matenk zenye kipenyo cha 3"-4" na mita 60 za malipo ya kabla zenye kipenyo cha 3/4"	38,765,600	51,000,000	30,750,000

10	Upanuzi wa mtandao wabomba yenye kipenyo cha mm63-mm50 urefu wa km 5.74 katika maeneo ya Samora,Majengo-batini,Kawawa Mji mwema Samora na Mbagala katika mwaka wa fedha 2019-2020 na pia upanuzi wa mtandao wa maji wenye urefu wa km4 katika eneo la ndurugumi kwa mwaka wa fedha 2020-2022	31,734,400	15,000,000	49,000,000
	Jumla ya ghrama za Uwekezaji mpya	93,500,000	119,000,000	109,750,000
	Jumla Kuu ya Gharama za Kukarabati, Kubadilisha, na Uwekezaji Mpya.	105,000,000	136,000,000	139,750,000

_____

JEDWALI LA TATU

_____

(Imetengenezwa chini ya Aya ya 4(b))

VIASHIRIA VYA UTENDAJI (2019/20 – 2021/22)

Maelezo	Unit	Lengo la Utendaji		
		2019/20	2020/21	2021/22
Kiwango cha idadi ya watu waishio kwenye mtandao wa maji	%	90	90	92
Kiwango cha upotevu wa maji	%	18	18	18
Ufanisi katika ukusanyaji wa mapato	%	90	95	98
Idadi ya watumishi kwa maunganisho 1000	/	8.2	8.2	7.8

_____

JEDWALI LA NNE

_____

(Imetengenezwa chini ya Aya ya 4(f))

GHARAMA ZILIZOIDHINISHWA

MAELEZO	MAKISIO (Shilingi)		
	2019/20	2020/21	2021/22
Uzalishaji	143,589,738	147,544,616	147,126,509
Usambazaji	69,250,000	73,062,500	77,115,625
Matengenezo	51,693,285	54,277,949	56,991,847
Utumishi	118,650,800	124,583,340	130,812,507

MAELEZO	MAKISIO (Shilingi)		
Utawala	68,465,942	71,889,239	75,483,701
Uhamasishaji wa Biashara	5,753,000	5,810,530	5,868,635
Matukio na Mikutano	3,850,000	3,922,620	3,826,173
Fedha	888,000	905,760	923,875
Bodi	8,400,000	8,400,000	8,400,000
Gharama za Uendeshaji na Matengenezo (Shilingi Milioni)	470,540,764	490,396,554	506,548,871
Uchakavu	130,198,196	130,198,196	130,198,196
Mahitaji yote ya Mapato (Shilingi Milioni)	600,738,960	620,594,750	636,747,067
TOA: Mapato Mengine (Shilingi Milioni)	11,715,110	12,300,866	12,669,891
Mahitaji ya Mapato toka Mauzo ya Maji (Shilingi Milioni)	589,023,850	608,293,885	624,077,175
Uzalishaji Maji (Milioni m3)	464,960	476,708	488,862
Upotevu wa Maji (%)	18%	18%	18%
Maji yanayouzwa (Million m3)	381,267	390,900	400,867
Bei ya Wastani (TZS/m3)	1,545	1,556	1,557

Dodoma
....., 2019

NZINYANGWA E. MCHANY
Mkurugenzi Mkuu